# Vijana watakiwa kuchangamkia fursa sekta ya mifugo, uvuvi

Na Mwandishi Maalumu

VIJANA wametakiwa kuchangamkia fursa zilizopo katika sekta za mifugo na uvuvi ili waweze kuzitumia kibiashara kujikomboa kimaisha.

Wito huo ulitolewa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alipotembelea banda la wizara hiyo katika Monesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), kwenye Viwanja ya Mwalimu JK Nyerere, Dar es Salaam.

"Vijana watumie maonesho haya kuja kujifunza fursa mbalimbali za kibiashara na za uwekezaji zinazopatikana katika sekta za mifugo na uvuvi kwa sababu Wizara ya Mifugo na Uvuvi mambo yake mengi ni ya uzalishaji na biashara."

"Kila kitu kilichopo katika wizara hii ni fursa katika biashara na ni fursa ya uwekezaji, hivyo tunawashauri vijana kutumia maonesho haya kujifunza na kutumia elimu watakayoipata kuboresha maisha yao huko wanakoishi," alisema.

Alisema katika banda la wizara hiyo kuna wataalamu mbalimbali ambao wanatoa elimu na mafunzo yanayohusu ufugaji na uvuvi ikiwamo ufugaji kuku, ng'ombe, mbuzi na samaki kibiashara.

"Kuna vijana wengi wanaotafuta kazi lakini hawajafanikiwa, hivyo nawashauri kwenda kujifunza fursa kubwa za kibiashara zitakazowasaidia kujipatia ajira na kukuza uchumi wa nchi.

Ulega alisema serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Samia Suluhu Hassan imejikita katika kufungua milango ya biashara na kuwataka wenye kiu ya kujifunza na kufanya kazi ya uzalishaji waende katika banda hilo ili waelimishwe jinsi kufanya kazi hiyo ambayo itakuwa na manufaa sio kwao tu bali kwa taifa pia.

Katika hatua nyingine, Ulega amezitaka taasisi zilizo chini ya wizara hiyo ikiwamo Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (Lita) na Wakala ya Mafunzo ya Uvuvi (Feta) kubuni mafunzo yatakayojumuisha watu wa elimu ya chini ambao wengi wao ni darasa la saba.

Alisema kwa sasa vijana wengi ambao hawajasoma wanakimbilia kuendesha bodaboda kwa maana ndio njia wanayoiona rahisi ya kujipatia kipato, huku akizitaka taasisi hizo kuja na mkakati maalumu wa kuanzisha mafunzo ya kuwafundisha vijana hao fursa zilizopo katika sekta hizo mbili na wakazitumia kujiajiri na kufanya uzalishaji mkubwa utakaowezesha hata nchi kupata mapato.

Habari leo Uk.17 , Julai 7, 2021

Scanned with CamScanner

Jumatano Julai 7, 2021 UHURU

# JUKWA LA UCHUMI



**KAHN KUBAKI MUNICH**
MKURUGENZI wa klabu ya Bayern Munich, Oliver Kahn anatarajia kumbakisha... **UK.22**

# Uwekezaji sekta ya mifugo mbinu bora kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana

**Na BARAKA LOSHILAA**

KUNDI kubwa la wafugaji Tanzania, linatafsiri ukubwa wa sekta hiyo na namna ambavyo hatuwezi kujisifu kama taifa bila kumtaja mfugaji.

Ndio maana unaposikia migogoro ya ardhi hapa nchini moja kwa moja inahusisha wakulima na wafugaji, ambao wanategemeana.

Wingi wao ndio huonyesha maisha halisi ya Mtanzania kama si mfugaji basi ni mkulima.

Makundi hayo ndio huifanya sekta za Mifugo, Uvuvi na Kilimo kushika nafasi muhimu katika ukuaji wa uchumi wa Taifa na kukuza pato la taifa.

Tukizungumzia sekta ya mifugo kulingana na uchambuzi wa sekta hiyo (LSA), unaonyesha Tanzania huchangia asilimia 1.4 ya ng'ombe waliopo duniani, huku kwa Afrika ikichangia asilimia 11 kwa mujibu wa Shirika la Kilimo Duniani (FAO) kwa 2014.

Takwimu hizo zimefanya Tanzania kuendelea kuboresha mikakati yake katika kuinua sekta ya mifugo iwe na tija kwa uchumi na maisha ya watu.

Mwaka 2020/2021 kwa takwimu ya Wizara ya Mifugo(Taarifa ya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, 2020), inaeleza idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka milioni 33.4 hadi milioni 33.9 kwa mwaka huu.

Pia, kuna ongezeko la mbuzi kutoka milioni 21.29 hadi milioni 24.5, kondoo milioni 5.65 hadi milioni 8.5, kuku milioni 87.7 wakiongezeka ikilinganishwa na takwimu za kuku milioni 83.28.

Licha ya ongezeko hilo, sekta ya mifugo kwa mwaka 2020 ukuaji wake ulikuwa kwa asilimia 5.0 huku mchango kwa pato la taifa likiwa ni asilimia 7.1 tofauti na 2019 ambapo mchango ulikuwa kwa asilimia 7.4.

Mchango huo, katika pato la taifa ni finyu ikilinganishwa na rasilimali za mifugo tulizonazo, ambazo hututambulisha katika ramani ya nchi tatu Afrika zenye kiwango kikubwa cha mifugo.

Ukubwa wa sekta hii duniani, hauna matumaini katika maisha ya watu hapa nchini kwa kuwa ukubwa wake haugusi mabadiliko ya walengwa na Taifa.

Tanzania inashika nafasi ya tatu kuwa na idadi kubwa ya mifugo barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudan, ambapo takwimu za mwaka 2018, mtandao wa Mamopanel unaonyesha, Ehiopia ina ng'ombe milioni 63, milioni 31 wakiwa mbuzi,milioni 33 kondoo na milioni 61 wakiwa ni kuku.



> **Katika idadi hiyo ya kuna ng'ombe bora wa maziwa milioni mbili tu. Hii ni asilimia ndogo ya ng'ombe bora wa maziwa na sababu kubwa hawapatikani kwa urahisi.**
>
> Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania (BTM), Dk. Geogre Msalya.

Wingi huo umechangia mchango mkubwa katika pato la taifa kwa asilimia 20 huku asilimia 20 ya fedha za kigeni katika taifa hilo zikitokana na mifugo, hiyo ikiwa ni takwimu za mwaka 2017.

Huku mataifa ya nje yakifurahia matunda yatokanayo na mifugo, Tanzania tunatumia fedha nyingi kuagiza maziwa nje huku tukiwa na tishio la uhaba wa nyama nyekundu.

Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania (BTM), Dk. Geogre Msalya, anasema hadi sasa tunazalisha lita milioni 5.4 ya maziwa kwa mwaka kutokana na ng'ombe milioni 33 waliopo.

"Katika idadi hiyo ya kuna ng'ombe bora wa maziwa milioni mbili tu. Hii ni asilimia ndogo ya ng'ombe bora wa maziwa na sababu kubwa hawapatikani kwa urahisi," anasema.

Msajili huyo anabainisha, ng'ombe bora wa maziwa hivi sasa ni gharama kubwa ambapo wamefikia sh. milioni 4.5 kwa ng'ombe mmoja tu anayetoa lita 20.

" Soko letu la ng'ombe wa maziwa limevamiwa na ng'ombe kutoka nchini Afrika Kusini. Wanauzwa dola 1800 sawa na zaidi ya sh. milioni 4.1" anasema.

Anasema uwepo huo unafanya gharama kubwa, ng'ombe waliopo ni wa asili wanatoa lita mbili hadi tano kwa siku hali hiyo, inachangia upungufu mkubwa wa maziwa, kulazimika kuagiza lita milioni 12 kutoka nje ya nchi katika kipindi cha miezi sita tu.

"Hii inagharimu siyo chini ya sh. bilioni 14 hadi 20 kwa mwaka. Tunapeleka fedha nje ya nchi wakati tuna mikono, tuna miguu na nguvu ya kuzalisha. Hivyo nawahimize wafugaji wawe wabunifu," anabainisha.

Kwa takwimu za Wizara ya Mifugo, viwanda vya maziwa vilivyopo ni ni 81 huku vikiwa na uwezo wa kusindika lita milioni 276.55, kwa mwaka.

Kwa sasa vinasindika lita milioni 56.25 kwa mwaka (sawa na asilimia 20.3).

Juhudi za serikali kuhakikisha rasilimali za mifugo zinakuwa na tija kwa wananchi na taifa kwa ujumla Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Mifugo imeweka Dira ya Maendeleo inayoendana na Dira ya Maendeleo Tanzania, ambayo inaeleza kufikia mwaka 2025.

"Kuwe na Sekta ya Mifugo ambayo ifikapo mwaka 2025 kwa sehemu kubwa, utahusisha ufugaji wa kisasa na endelevu, uwepo wa mifugo bora, uzalishaji mzuri, utakaoendeshwa kibiashara lengo kuboresha lishe ya Mtanzania,kuinua kipato cha mfugaji, Taifa na kuhifadhi mazingira.

Dhamira ya sekta ya mifugo ni kuhakikisha rasilimali za mifugo zinaendelezwa na kutunzwa katika mazingira endelevu, kwa ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi

Mbali na kuwa na sera yenye mipango bora kwa ukuaji wa sekta ya mifugo bado tuna Mpango kabambe wa sekta hiyo ya mwaka 2017/2018-2021-2022, ambayo inaeleza.

Sekta ya mifugo ina umuhimu mkubwa kujenga uchumi imara, kuongeza kipato na fursa za ajira nchini.

Awamu ya kwanza ya mpango huo unakadiria ongezeko la ajira ya watu milioni mbili watakaojishughulisha na ufugaji.

Kutokana na tathmini, dira hiyo inaonyesha kwa miaka 15 ijayo (kufikia mwaka 2032) nchi itakumbwa na uhaba mkubwa wa nyama hasa nyama nyekundu kiasi cha tani 1,731,000 sawa na upungufu wa asilimia 33 ya mahitaji.

Hivyo kama hakutakuwa na juhudi za ziada za kuongeza uwekezaji, Tanzania itakuwa na upungufu mkubwa wa bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo hivyo kulazimika kuagiza kutoka nje ya nchi.

Haya yanaonyesha licha ya umuhimu wa mifugo na mipango mizuri ambayo serikali imeweka, bado msukumo wa kiutendaji ni hafifu kuonyesha matokeo ya namna sekta hii inavyoleta tija kwa wananchi.

Wafugaji wengi kwa sasa wanafuga kupata mlo wa siku hali yao ya maisha ikibaki katika mazingira ya kuswaga ng'ombe machungani asubuhi na kuwarejesha jioni.

Kukosekana kwa mipango madhubuti tunashindwa kuchangamkia fursa zilizopo katika sekta ya mifugo hivyo tunaamini ajira pekee tunayopaswa kuwa nayo ni kukaa ofisini.

Fursa isipotengenezewa njia na mamlaka husika,wengi tutaiogopa kwa kuamini kuwa kuitumia ni sawa na kupoteza muda.

Tunapoamua kuchukua hatua kuboresha sekta ya mifugo tutazame bajeti inayotengwa na serikali ni kwa namna inawasaidia wakulima kupiga hatua kutoka walipokuwa jana kwenda mbele zaidi.

Pia, namna watakavyoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika ufugaji na kuachana na zama za kuwa na mifugo mingi wasio na tija.

Bajeti pekee ambayo serikali imetenga kwa sekta ya mifugo ni sh. bilioni 47,844,949,810 kwa mwaka 2021, 2021.

Kwa mwaka ujao wa fedha, ni vyema serikali ikangalia sekta hiyo kwa ukubwa wake na kutenga kiwango kikubwa cha fedha, yenye kugusa maisha ya kila mfugaji tofauti na sasa ambavyo bado jamii ya wamasai wanaona ufahari kuwa na mifugo mingi huku maisha yao yakiwa duni.

Tukithamini sekta ya mifugo na kufanya uwekezaji wa kutosha, tunatengeneza njia sahihi ya kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana wetu na kuepusha ufahari wa kumiliki mifugo mingi isio na tija.

Pia, ni wakati sasa serikali kuangalia mipango iliyo katika wizara husika ili fedha zinazotengwa ikatoe nafasi ya utekelezaji wa yale yaliyoandikwa katika makaratasi.

Mbali na hilo katika jamii zetu kundi kubwa la wanawake na vijana ndio hujihusisha na ufugaji hivyo lazima kama nchi tuwe na mikakati ya namna kundi hili litakavyoshiriki katika mnyororo wa thamani wa mifugo.

Hadi sera za mifugo, haielezi dhahiri ni kwa jinsi gani wanawake wanawezeshwa kushiriki kiufanisi katika sekta hii.

Ushirikishwaji wa wanawake na vijana katika mnyororo wa thamani wa mifugo, hautaishia kuboresha maisha yao tu, bali utachangia kufikia malengo ya taifa ya uhakika wa chakula na lishe bora.

Kutokana na mipango isiyotekelezeka licha ya kuwa na wingi wa mifugo bado tunaagiza maziwa kutoka nje ya nchi huku kukiwa na tishio la upungufu wa nyama nyekundu.

Maboresho ya sekta ya mifugo nchini ni muhimu yafanyike kuongeza tija, kwani pamoja na kuwa na sera nzuri bado tunalega lega kuyafanya kazi yale tuliyoyakubali.



UFUGAJI kwa njia ya kisasa



NJIA za asili za ufugaji

Scanned with CamScanner

Habari Leo uk.17 .Julai 7,2021

# Wafugaji Arusha wanufaika dawa ya kutibu ngozi

Na Lucy Ngowi

WAFUGAJI 400 mkoani Arusha wamefikiwa na dawa ya kutibu ngozi na kuongeza thamani ya bidhaa hiyo ili kupata masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mhadhiri wa Chuo cha Wanyamapori (Mweka), Dk Never Mwambela alisema hayo katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) yanayoendelea kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Alisema bidhaa hiyo aliyoitafiti iliyopewa jina la VB, imewawezesha wafugaji hao kuona thamani ya ngozi za mifugo yao tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa wakizitupa kwa kuwa hazikuwa na soko.

Alisema ngozi ikitunzwa vizuri inaweza kuwa na thamani kubwa kuliko nyama yenyewe.

Alisema bidhaa hiyo aliitafiti baada ya kupata ufadhili wa Sh milioni 70 kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech) na imewasaidia wafugaji 400 wa mkoani Arusha kuongeza thamani ya ngozi za mifugo yao.

"Tanzania ni ya pili barani Afrika kwa kuwa na mifugo mingi lakini wananchi wake bado ni maskini. Ukipita mikoa wanayofuga kama Mwanza, Shinyanga na Arusha ngozi nyingi zinatupwa hazina soko," alisema.

Alisema wafugaji hao 400 kutoka wilaya za Arusha, Monduli na Longido walitumia bidhaa hiyo hivyo wametunza ngozi nyingi ila changamoto yao kubwa ni viwanda vya kuchakata ngozi ni vichache.

Scanned with CamScanner

# Uhuru Uk.16, Julai 7, 2021

## MALISHO



**NAIBU** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah [illegible], akiangalia mbegu za malisho aina ya Juncao zinazozalishwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI), katika [illegible], wakati wa Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, katika viwanja vya Mwalimu Nyerere, [illegible].

Scanned with CamScanner